22/1/2002

# wakulima na wafugaji

## *uimarishaji wa mahusiano*





Warsha ya Tatu ya Wakulima wa Kanda ya Mashariki

iliyofanyika Mjini Bagamoyo,
Tarehe 8 - 11 Oktoba 2001

**TARP II - SUA Project**

Mwenendo wa Warsha ya Tatu ya
Wakulima wa Kanda ya Mashariki Kuhusu

# Mahusiano Baina ya Wakulima na Wafugaji

Iliyofanyika Mjini Bagamoyo
Tarehe 8 – 11 Oktoba 2001

Warsha hii ilitayarishwa na
Kamati ya Utekelezaji ya
Mradi wa
**Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa**
**Wakulima Wadogowadogo Tanzania:**
Mradi wa Utafiti Unaotilia Mkazo Wanawake

Mradi huu upo chini ya
Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili
(TARP II – SUA Project)

*Imetayarishwa na*

A. M. Bakari

*Na Kuhaririwa na*

Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B Kinabo | Mratibu |
| Dk. (Bi.) J. Lyimo Macha | Mjumbe |
| Prof. R.E. Malimbwi | Mjumbe |
| Prof. E.K. Batamuzi | Mjumbe |
| Prof. A.J. Tarimo | Mjumbe |
| Dr. P.J. Makungu | Mjumbe |

**ISBN: 9987 605 51 6**

***Kimechapishwa na:***

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima
Wadogowadogo Tanzania (TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo namba: TS 2-31

© TARP II – SUA Project 2001

# YALIYOMO

**Dibaji**......................................................................v
**Vifupisho**......................................................................vi
**Muhtasari**......................................................................vii

**1. UTANGULIZI** ...................................................................... 1

**1.1 Maandalizi na uendeshaji** ...................................................................... 1

**1.2 Madhumuni** ...................................................................... 1

**2. MWENENDO WA WARSHA** ...................................................................... 1

**2.1 Utambulisho na Ufunguzi** ...................................................................... 1

**2.2 Kutathmini mahusiano baina ya wafugaji na wakulima wa mazao** ... 2

**2.3 Maelezo kuhusu mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo** ........... 5

2.4 **Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi**.................... 5

2.4.1 Matatizo yanayohusu matumizi ya ardhi na maji ................ 6

2.4.2 Matatizo yanayohusu utendaji wa viongozi na serikali ........ 8

2.4.3 Matatizo ya kijamii........................................................ 10

**2.5 Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi**.................... 11

2.5.1 Kikundi cha wakulima kutoka Doma na Lugoba ............... 11

2.5.2 Wafugaji wa Bagamoyo................................................ 12

2.5.3 Wakulima wa Ludewa na Mvumi ...................................... 12

2.5.4 Wafugaji wa Morogoro vijijini ........................................ 13

2.5.5 Watendaji waandamizi wa wilaya ..................................... 13

**3. MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI, MIKAKATI YAKE NA WAHUSIKA KATIKA UTEKELEZAJI**.................................... 14

**3.1 Utatuzi wa rushwa** ...................................................................... 14

3.1.1 Kuboresha mazingira ya watumishi wa serikali .................. 14

3.1.2 Kupanua uelewa wa wananchi juu ya haki zao .................... 15

3.1.3 Kukuza uwezo wa wananchi kufuatilia haki zao................... 15

3.1.4 Kuimarisha usimamizi na utekellezaji wa sheria ya rushwa... 16

**3.2 Utatuzi wa kuondoa tofauti za mitazamo ya kimila**................... 16

3.2.1 Mamlaka za kimila ziondoe tofauti zao ............................. 16

**3.3 Utatuzi wa upungufu wa ardhi, malisho na maji kwa ajili ya kilimo na mifugo** ........ 16

3.3.1 Kuboresha mazingira ya watumishi wa serikali ........ 16

3.3.2 Kuweka uwiano sahihi wa ardhi, maji, mifugo na mazao ........ 16

3.3.3 Kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua ........ 17

**3.4 Ufumbuzi wa mikakati hafifu katika matumizi ya ardhi na maji kwa ajili ya kilimo na mifugo** ........ 17

3.4.1 Kuweka mikakati itakayo hakikisha matumizi bora na sahihi ya matumizi ya maji na ardhi ........ 17

**4. HITIMISHO** ........ 17

**4.1 Tamko la warsha** ........ 17

**4.2 Kufunga** ........ 18

VIAMBATANISHO 19

Kiambatanisho Namba 1: Orodha ya Washiriki ........ 19

Kiambatanisho Namba 2: Kielelezo cha mfano hai wa ajali nyingi Barabarani ........ .20

Kiambatanisho Namba 3: Michoro inayoonesha uhusiano wa matatizo, viini vyake, na kipaumbele katika utatuzi wa kila kiini ........ 21

# DIBAJI

Chapisho hili linawasilisha Mwenendo wa Warsha ya Tatu ya Wakulima wa Kanda ya Mashariki kuhusu uimarishaji wa mahusiano yaliyopo baina ya wakulima wa mazao na wafugaji. Warsha ilifanyika katika Chuo cha Uongozi wa Elimu (MANTEP) Mjini Bagamoyo tarehe 8 hadi 10 Oktoba 2001.

Warsha hii ni moja ya warsha ambazo zimepangwa kufanyika kama shughuli muhimu za kuutekeleza mradi wa **Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania**. Mradi huu ambao ulianza rasmi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD), na unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo. Warsha hizi zina madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo na washika dau wengine ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo.
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo.
3. Kudadisi ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi.
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

Kamati ya Utekelezaji wa Mradi inatarajia kuwa chapisho hili litakuwa la manufaa kwa washika dau mbalimbali, na mapendekezo yaliyotolewa na washiriki wa warsha yatachangia katika juhudi za kuimarisha uhakika wa chakula nchini.

*L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

*Novemba 2001*

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| NLH | Agricultural University of Norway (*Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo*) |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation (*Shirikia la Maendeleo la Norway)* |
| SUA | Sokoine University of Agriculture (*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo*) |
| TARP II | Tanzania Agricultural Research Project Phase Two ( *Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili*) |
| MANTEP | Management Training in Education Programmes |
| PFM | Participatory Farm Management |



*Washiriki wa warsha wakiwa kwenye picha ya pamoja*

# MUHTASARI

Warsha ilishirikisha wakulima wa mazao, wafugaji, wataalamu wa ugani, watafiti na watumishi waandamizi katika idara za kilimo, mifugo, ardhi na mipango kutoka wilaya za Kilosa, Bagamoyo na Morogoro vijijini. Lengo kuu la warsha lilikuwa ni kutafakari vyanzo vya migogoro baina ya wafugaji na wakulima inayotokea katika wilaya hizo na hatimaye kubaini mbinu muafaka katika kuepuka migogoro hiyo na kupendekeza mikakati ya namna ya kuitatua.

Washiriki wa warsha waliridhika kuwa mahusiano baina ya wakulima na wafugaji katika wilaya zao ni mabaya. Mahusiano mazuri pekee yaliyopo baina ya wakulima na wafugaji ni katika kuuziana bidhaa.

Mazingira muhimu katika migogoro baina ya wafugaji na wakulima katika wilaya hizo ni wafugaji wasio na asili ya kilimo cha mazao kuishi pamoja na wakulima wasio na asili ya ufugaji. Hata hivyo wafugaji wa jamii ya kimasai wanakabiliwa zaidi na migogoro baina yao na jamii za wakulima wa mazao ikilinganishwa na jamii zingine za wafugaji.

Mwingiliano katika matumizi ya ardhi na maji unaotokana na uwiano mbaya uliopo wa matumizi ya rasilimali hizo katika shughuli za ufugaji na kilimo cha mazao ni chanzo cha msingi wa migogoro. Vyanzo muhimu vya kutokuwepo kwa uwiano sahihi wa matumizi ya ardhi na maji ni:

- ◊ Kutokuwepo kwa mipango ya kitaifa ya matumizi ya ardhi na maji kwa uwiano sahihi katika ufugaji na kilimo cha mazao,
- ◊ Sheria dhaifu na zisizosimamiwa kikamilifu juu ya udhibiti wa matumizi bora ya raslimali. Vyombo vya dola hutumia mwanya wa udhaifu wa sheria zilizopo na uelewa mdogo wa haki walionao wafugaji na wakulima kupoteza haki za waathirika wa migogoro hali ambayo inatafsiriwa kuwa ni kukithiri kwa rushwa miongoni mwa watendaji wa serikali. Hali hiyo imepelekea waathirika wa migogoro kukatishwa tamaa na utendaji wa vyombo vya dola na kujichukulia sheria mikononi mwao.

Tofauti kubwa ya mila na desturi iliyopo baina ya wafugaji na wakulima wa mazao katika maeneo yenye migogoro imesababisha kudharauliana kijamii na kiuchumi na hivyo kujenga chuki miongoni mwa jamii. Chuki hiyo imeondoa uwezekano wa kusuluhisha kijamii migogoro inayotokea baina yao.

Mbinu hafifu katika kilimo cha mazao na ufugaji pia zinachangia katika kutokuwa na uwiano mzuri wa matumizi ya ardhi na maji. Wakulima na wafugaji hawatumii utaalamu wa kutosha juu ya mbinu bora na endelevu. Hata wale wachache wanaojua umuhimu wa kutumia mbinu bora wanashindwa kutumia mbinu hizo kwa sababu ardhi wanayotumia hawana haki kisheria juu yake. Ilionekana kuwa ni vigumu mfugaji kuchukua jukumu la kuhifadhi malisho kwenye eneo ambalo kila mfugaji anaweza kuchungia na wakati maeneo ya kuhamishia mifugo yakiweko. Aidha ni vigumu mkulima wa mazao kuhifadhi rutuba wakati kijiji au serikali kuu inaweza kuamua kulitumia eneo hili vinginevyo wakati wowote. na pia yako maeneo mengine ya kufungua mashamba mapya yenye rutuba.

Ufumbuzi wa kuondoa migogoro ulilenga kwanza katika kuondoa tatizo la rushwa ili sheria zilizopo zitekelezwe kikamilifu. Mikakati iliyopendekezwa ni kuboresha mazingira ya watumishi wa vyombo vya dola, kuwepo kwa sheria zinazokidhi mahitaji ya wakati huo na zinazotekelezeka. Aidha kuinua uelewa wa haki na kukuza uwezo wa wananchi kukataa kupotezewa haki zao ni moja ya mikakati hiyo. Serikali, mashirika

yasiyo ya kiserikali na wananchi wenyewe walitakiwa kuwajibika katika utekelezaji wa mikakati hiyo. Aidha wananchi walitakiwa kuondoa chuki iliyojengeka miongoni mwao ili waweze kuunda mamlaka za kimila zinazokubalika pande zote ili migogoro iwe inamalizwa kijamii ambako mwanya wa rushwa haupo.

Ufumbuzi mwingine ulilenga katika udhibiti wa matumizi ya ardhi na maji kwa uwiano sahihi baina ya mifugo na kilimo cha mazao. Serikali ilitakiwa kuwashirikisha kikamilifu wafugaji, wakulima, wataalamu wa fani zote zinazohusika na washika dau wengine ili kubuni mipango sahihi na inayotekelezeka ya kitaifa ya kudhibiti matumizi holela ya ardhi na maji. Msisitizo uliwekwa juu ya kuhimiza na kuwezesha matumizi ya mbinu bora na endelevu katika ufugaji na kilimo cha mazao.

Tamko la warsha hiyo lilisisitiza ufuatiliaji na utekelezwaji wa maazimio ya warsha za aina hiyo bila kungoja mifumuko ya migogoro yenye madhara makubwa kwa watu na mali zao.



*Baadhi ya washiriki wa warsha wakiwa kwenye zoezi la kutambua viini vya matatizo*

# 1 UTANGULIZI

### *1.1 Maandalizi na uendeshaji*

Warsha juu ya mahusiano baina ya wakulima na wafugaji wa Kanda ya Mashariki iliandaliwa na mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo (TARP II SUA) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Warsha ilifanyika katika Chuo cha Uongozi wa Elimu (MANTEP) Mjini Bagamoyo. Walioshiriki katika warsha hiyo ni wafugaji na wakulima 17 kutoka katika wilaya za Kilosa, Morogoro vijijini na Bagamoyo. Kati yao wafugaji walikuwa 9 na wakulima 8. Wanawake walikuwa 4 na wanaume 13. Washiriki wengine walikuwa mtafiti 1 kutoka kituo cha Utafiti cha Ilonga, Kilosa, 1 kutoka kituo cha Utafiti wa Mifugo, Tanga na wengine 2 kutoka SUA. Wengine walioshiriki ni Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya ya Bagamoyo, Afisa kutoka Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Kilosa, Afisa Mipango wa Wilaya ya Kilosa na wataalamu wa ugani 5 kutoka maeneo yote waliyotoka wakulima. Orodha na wasifu wa washiriki upo kwenye Kiambatisho Na. 1.

Washiriki wa warsha hiyo walitoka kwenye maeneo yenye migogoro baina ya wafugaji na wakulima wa mazao katika Kanda ya Mashariki. Taarifa za mapigano baina ya wakulima wa mazao na wafugaji zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara kutokea katika maeneo hayo. Umwagaji damu, upotevu wa maisha ya watu na mali vimeripotiwa kutokea katika migogoro na mapigano hayo. Hali hii inaashiria ukosefu wa amani na utulivu katika jamii za maeneo hayo. Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato Katika Kaya unaamini kuwa utulivu na amani ni nguzo muhimu katika kuifanya jamii kuwa na uhakika wa chakula na kipato. Hivyo, Mradi ulichukua jukumu la kuendesha warsha hii kama moja ya mikakati yake katika kutimiza malengo yake.

### *1.2 Madhumuni*

Lengo kuu la warsha hiyo lilikuwa ni kutafakari vyanzo vya machafuko baina ya wafugaji na wakulima katika wilaya za Kilosa, Morogoro vijijini, na Bagamoyo na kubaini mbinu muafaka katika kuepuka migogoro hiyo. Hivyo, warsha ilikuwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kubainisha mahusiano yalivyo hivi sasa baina ya wakulima na wafugaji katika wilaya zilizowakilishwa kwenye warsha na kuainisha shida kuu iliyopo

ii. Kubainisha sababu za kuwepo kwa shida hiyo kuu, viini vyake na umuhimu wake katika kupewa kipaumbele

iii. Kupendekeza ufumbuzi, mikakati na wahusika katika utekelezaji wa mapendekezo

# 2 Muundo wa warsha

### *2.1 Utambulisho na ufunguzi*

Washiriki waliwasili kwenye ukumbi wa warsha saa 2.30 asubuhi tarehe 8/10/2001. Washiriki walijitambulisha kwa majina, walikotokea na wasifu wao (Kiambatanisho Na.

1). Baada ya utambulisho washiriki walieleza matarajio yao kwa kuandika katika kadi. Matarajio ya washiriki yalikuwa ya aina kuu mbili kama ifuatavyo:

i. Kuboresha uzalishaji wa mazao na mifugo
   - Kujifunza mbinu ya uzalishaji wa mifugo na kilimo
   - Matumizi ya mbolea
   - Kubadilishana uzoefu na watu wengine kuhusu kilimo na ufugaji
   - Kujifunza kwa mjadala mafanikio na matatizo ya sehemu tofauti walikotoka
   - Kubadilishana mbinu za kitaalamu
   - Kuongeza elimu ya kilimo
   - Kujua maana ya Warsha

ii. Kuboresha mahusiano baina ya wakulima na wafugaji
   - Kuboresha mahusiano
   - Kuelewa sababu za ugomvi wa mara kwa mara
   - Kupata uwiano mzuri wa kilimo na mifugo
   - Kupata ufumbuzi wa matatizo ya wakulima na wafugaji
   - Kujua mahusiano kati ya mifugo na mimea
   - Muafaka juu ya matumizi ya ardhi
   - Kupata suluhisho la kudumu kati ya wakulima na wafugaji
   - Kuelewa njia za kutatua migogoro kati ya wafugaji na wakulima

Hatimaye Mgeni rasmi Dk. Materu, J. A. ambaye pia ni Afisa wa Kilimo na Mifugo wa wilaya ya Bagamoyo aliwasili kwenye ukumbi wa warsha. Kaimu Mratibu wa Mradi Profesa Emanuel Batamuzi alimkaribisha mgeni na kumtambulisha kwa washiriki. Kaimu wa Mratibu wa mradi alimfahamisha mgeni rasmi pamoja na washiriki lengo na madhumuni ya Mradi. Baadaye alimkaribisha mgeni rasmi kuzungumza na washiriki.

Katika hotuba yake mgeni rasmi aliwasisitizia washiriki wa warsha kutumia fulsa zinazotolewa na Mradi huo ili kuwawezesha watafiti wa SUA na wale wa wizara ya kilimo kufanya tafiti ambazo zitaleta matunda haraka iwezekanavyo. Mgeni rasmi aliifungua warsha rasmi na kupiga picha ya pamoja na washiriki.

### *2.2 Kutathmini mahusiano baina ya wafugaji wa wakulima wa mazao*

Shughuli hiyo ilifanyika katika vikundi. Washiriki walipendekeza vigezo vifuatavyo katika kugawanyika kwenye vikundi.

i. Kutamka namba
ii. Idadi sawa ya makundi tofauti yaliyowakilishwa kwenye warsha
iii. Kufuata jinsia
iv. Uwiano wa maeneo yaliyowakilishwa
v. Kila kundi lililowakilishwa yaani wakulima wa mazao, wafugaji na wataalamu kuwa peke yao.

Washiriki waliafikiana kugawanyika kwa kufuata kigezo Na. V na hivyo kupata vikundi vitatu ambavyo ni:

- wakulima wa mazao,

- wafugaji
- wataalamu (watafiti, washauri wa ugani na maafisa waandamiza wa wilaya).

Sababu kubwa iliyopelekea washiriki kugawanyika kwa kigezo hicho ni kuwa kila kundi lililowakilishwa baina ya makundi hayo matatu lipate wasaa na uhuru wa kotosha kueleza bayana hali ilivyo kwa mtazamo wao wenyewe.

Dondoo zilizotumiwa na washiriki katika majadiliano ya vikundi ni:

- Mahusiano gani mazuri yaliyopo baina ya mkulima na mfugaji?
- Mahusiano gani yasiyoridhisha yaliyopo baina ya mkulima na mfugaji?
- Mahusiano gani yasiyokuwepo ambayo yangepaswa kuwapo?

Vikundi viliwasilisha matokeo ya majadiliano yao kama ifuatavyo:

i. Kikundi cha wafugaji

*Mahusiano mazuri*

- Wakulima kununua bidhaa za mfugaji (maziwa, nyama na mbolea)
- Kupata (kununua) chakula kama mahindi na matunda
- Kutembeleana

*Mahusiano mabaya*

- Wakulima kulima sehemu za malisho
- Wakulima kuwachukia wafugaji
- Hakuna urafiki wa kweli

*Mahusiano yanayotarajiwa*

- Mgawanyo mzuri wa ardhi
- Mahusiano kijinsia yaani kuoleana
- Kuheshimiwa kwa mipaka ya maeneo yanayokidhi mahitaji (malisho/kilimo)

ii. Kikundi cha wakulima wa mazao

*Mahusiano mazuri*

- Kupata maziwa na nyama
- Kupata mbolea
- Kuuza mazao

*Mahusiano yasiyoridhisha*

- Uharibifu wa mazao
- Kutoshirikiana katika shida kama misiba
- Kutoheshimu maeneo ya kilimo
- Uchungaji holela wa mifugo
- Kuwa na mifugo mingi kuliko uwezo wa eneo

*Mahusiano yanayotarajiwa*

- Kushirikiana wakati wa shida
- Kukubali na kuheshimu maeneo yaliyotengwa
- Kuelimishana kijamii ili kudumisha amani

iii. Kikundi cha wataalamu wanavyo yaona mahusiano baina ya wakulima na wafugaji

*Mahusiano mazuri*

- Mkulima kupata bidhaa za mifugo
- Kupata ajira hasa kuchunga
- Kupata soko la mazao
- Mfugaji kupata chakula
- Malisho kutokana na masalio ya mazao
- Kupata soko la bidhaa za mifugo

*Mahusiano mabaya*

- Uharibifu wa mazao
- Uharibifu wa ardhi, kuhamisha mbolea na kugandamiza ardhi
- Kiburi cha wafugaji
- Kutothamini ajira ya mtu
- Mapigano
- Ugandamizaji kijamii
- Upanuzi wa maeneo ya kilimo bila mpangilio
- Ulimaji kwenye vyanzo vya maji

*Mahusiano yanayopaswa kuwepo*

- Kuheshimiana
- Kuwepo uongozi wa pamoja baina ya wakulima na wafugaji
- Kuwepo kamati ya usuluhishi
- Yatengwe maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji
- Kuwepo kwa njia za mifugo vijijini kama ilivyo kitaifa
- Mipaka ya vijiji iheshimiwe
- Kuboresha mifugo bila kuongeza idadi
- Kilimo na ufugaji vizuiwe katika vyanzo vya maji
- Kutoa huduma za mifugo vijijini
- Sheria zilizopo ziheshimiwe

Kwa mtazamo wa wakulima na wataalamu kuhusu mahusiano, mazuri yaliyopo baina ya wakulima na wafugaji ni ya kiuchumi pekee, yaani kuuziana bidhaa. Wafugaji wao waliona kuwa pamoja na mahusiano mazuri yaliyopo ya kiuchumi, wanathamini pia hali iliyopo ya kutembeleana.

Vikundi vyote vilionesha kuwa mahusiano mabaya yaliyopo baina ya wakulima na wafugaji ni yale yanayohusu mahusiano katika matumizi ya rasilimali hasa ardhi na mahusiano ya kijamii. Vikundi vyote havikuweza kujibu sawasawa dondoo ya tatu kuhusu mahusiano yaliyokosekana ambayo wangependa yawepo. Kila kikundi kiliorodhesha zaidi ufumbuzi wa mahusiano mabaya ambao ulishughulikiwa katika vipindi vya warsha vilivyofuata.

Baada ya majadiliano washiriki waliafikiana kuwa hali ya mahusiano kati ya wakulima na wafugaji ni MABAYA. Ijapokuwa wanategemeana kiuchumi, lakini iwapo maisha yao kijamii hayatengamani basi migogoro haitakosa kuwepo, na hiyo ndiyo shida kuu iliyopo katika jamii hizo zilizotoka katika wilaya zilizowakilishwa kwenye warsha.

Wakati wa majadiliano washiriki walijiuliza swali jingine kuwa: Je, kila mahali ambako wakulima na wafugaji wanaishi pamoja kuna migogoro? Washiriki walitoa jibu kuwa siyo kila mahali pana migogoro. Walitoa mifano ya mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Dodoma, Arusha na Singida. Japokuwa mikoa hiyo ina wafugaji na wakulima wengi zaidi ya sehemu zingine nchini hakuna migogoro baina yao kama ilivyo katika wilaya zilizowakilishwa kwenye warsha. Uchambuzi wa swala hilo ulibaini kuwa maeneo yote yenye migogoro baina ya wafugaji na wakulima yana sifa moja au zaidi kati ya sifa zifuatazo:

i. *Maeneo mapya*

Wakulima na wafugaji wamekutana maeneo ambayo hapo awali hayakuwa ya wafugaji wala wakulima. Maeneo hayo ni kama yaliyokuwa mashamba makubwa ya umma, mbuga na misitu iliyokuwa haikaliwi na watu kama ile ya Bagamoyo.

ii. *Maeneo ya asili ya wakulima*

Maeneo ambayo wakulima waliwakaribisha wafugaji (ambao asili yao siyo kulima mazao).

iii. *Mashamba ndani ya maeneo ambayo asili yake ni malisho*

Maeneo ambayo wafugaji walikuwepo kwanza baadaye wakulima kufungua mashamba ndani ya maeneo hayo.

Washiriki pia walijiuliza swali jingine: Je, migogoro inatokea kwa jamii zote za wafugaji na wakulima? Uchambuzi ulionesha kuwa migogoro hutokea zaidi pale ambapo wafugaji wasio na asili ya kilimo kuishi pamoja na wakulima wasio na asili ya kufuga. Uchambuzi ulionesha pia kuwa jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai ndiyo yenye kukumbwa na migogoro zaidi ukilinganisha na jamii zingine za wafugaji kama vile Wabarbaig. Hata hivyo tofauti za itikadi ya mila na desturi ni mazingira muhimu ya migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

### *2.3 Maelezo kuhusu mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo*

Baada ya shida kuu kujulikana washiriki walijifunza kwa ufupi kuhusu mbinu ya ufumbuzi yakinifu wa matatizo. Mbinu ambayo wangeitumia katika kutafuta sababu za kuwepo kwa tatizo kuu lililobainishwa, viini vyake na umuhimu wake. Mada hiyo ilifundishwa kwa kutumia kielelezo cha mfano hai wa shida ya **ajali nyingi za barabarani** (Kiambatisho Na. 2). Baada ya washiriki kuonesha kuwa wameielewa mbinu hiyo waliendelea na hatua zilizofuata.

### *2.4 Kubainisha matatizo, jinsi yanavyohusiana na umuhimu wake katika kipaumbele*

Washiriki walikubaliana kuendelea na mgawanyo wa vikundi kama ilivyokuwa awali. Hata hivyo ilionekana kuwa ili zoezi hilo lifanyike kwa makini na ufasaha zaidi washiriki wakulima na wafugaji waligawanyika tena katika vikundi. Pia washauri wa ugani na watafiti waliungana na wakulima ama wafugaji kufuata maeneo wanayotoka na taaluma walizobobea. Maafisa waandamizi walibakia katika kikundi chao peke yao. Kutokana na makubaliano hayo vikundi vitano vilitokea. Vikundi viwili vya wakulima, viwili vya wafugaji na kimoja cha wataalamu waandamizi wa wilaya.

Katika majadiliano kwenye vikundi, washiriki walitumia mbinu ya utatuzi yakinifu. Waliainisha sababu za tatizo kuu na kuweka katika michoro jinsi matatizo hayo yanavyohusiana. Kila kikundi kiliwasilisha matokeo yake katika michoro hiyo na kujadiliwa na wanawarsha wote. Majadiliano yalilenga katika kupata ufafanuzi wa jinsi wanakikundi walivyofikia maamuzi yao. Hatimaye washiriki walirudi katika vikundi vyao ili kupatia kipaumbele viini vya matatizo waliyoainisha. Walitumia mbinu ya utatuzi yakinifu kufanya zoezi hilo. Kila kikundi kiliwasilisha matokeo ya kazi yake kwa washiriki wote na kujadiliwa. Orodha ya viini vya tatizo kuu na kipaumbele ilipatikana kwa kila kikundi.

Kwa ujumla matatizo chanzo na viini vya tatizo kuu yalikuwa yanafanana katika makundi yote japokuwa kila kundi lilikuwa na mtazamo wake kuhusu matatizo hayo. Matatizo hayo yamegawanyika katika matabaka matatu yanayohusu:

i. Matumizi ya rasilimali hasa ardhi na maji

ii. Utendaji wa viongozi na serikali

iii. Tofauti za kijamii

Matatizo hayo yanaripotiwa pamoja na mitazamo ya kila kundi lililowakilishwa kwenye warsha.

### 2.4.1 Matatizo yanayohusu matumizi ya ardhi na maji

Ilionekana kuwa matatizo yanayohusu matumizi ya maliasili hasa ardhi na maji ndiyo kitovu cha migogoro yote iliyoko baina ya wafugaji na wakulima. Kwa kawaida mifugo na mazao vinapozalishwa katika eneo lilelile kwa wakati mmoja hasa katika mifumo ya asili, huwepo ushindani wa matumizi ya ardhi na maji kati ya mifugo na mazao. Mitafaruku hutokea baina ya wafugaji na wakulima hasa pale unapotokea uharibifu ama wa mifugo kuathiriwa na madawa ya shambani au mifugo kulishwa mazao ya mkulima. Matatizo hayo yanayohusiana na matumizi ya ardhi na maji ni kama ifuatavyo:

i. *Kuingiliana katika matumizi ya ardhi na maji.*

Mtazamo wa **wafugaji** ni kuwa wakulima wamekuwa wakivamia maeneo ya malisho na kufungua mashamba yao bila kujali kuwa maeneo hayo ni ya malisho ya wanyama. Pia wamekuwa wakilima kando ya vyanzo vya maji au katika njia zinazoelekea malishoni au katika vyanzo vya maji ambako wafugaji hunywesha mifugo yao. Hali hiyo imepelekea mifugo kulazimika kuingia katika mashamba yenye mazao wakati ikielekea kwenye malisho au kunyweshwa maji.

Kwa upande wao **wakulima** wanaona kuwa wafugaji hupitisha mifugo yao au huchungia mahali popote ili mradi wanapata mahitaji ya mifugo bila kujali hata kama sehemu wanakopita au kulisha mifugo kuna mazao yanayoweza kuharibiwa.

Mtazamo wa wataalamu na wanawarsha wote kwa ujumla ni kuwa hali ya muingiliano ipo kwa kila upande, mfugaji kumuingilia mkulima na mkulima kumwingilia mfugaji.

ii. *Ukosefu wa mipaka*

Makundi yote yaliyowakilishwa kwenye warsha yalikuwa na mtazamo sawa juu ya tatizo hili. Vijiji vingi havina mipaka inayoeleweka. Hata pale ambapo kijiji cha

wafugaji na kile cha wakulima vimepakana yapo maeneo ambayo kila upande unaona kuwa ni haki yake kuyatumia. Hali hiyo husababisha muingiliano ambao hatimaye ni uhasama.

iii. *Kutoheshimu mipaka*

Wanawarsha walikuwa na mtizamo wa aina moja juu ya tatizo hilo. Walikubaliana kuwa hata pale ambapo mipaka inaeleweka mipaka haiheshimiwi. Wakulima hufungua mashamba katika maeneo ya malisho na wafugaji kuchungia kwenye maeneo ya mashamba huku kila mmoja akijua kuwa hapaswi kuingia. Hali hii pia hutokana na **uvamizi wa ardhi kwa mabavu** unaotokana na **ukorofi** wa baadhi ya wakulima au wafugaji.

iv. *Ukosefu wa hati miliki*

Vijiji kutokuwa na hati miliki kunawafanya wanakijiji waonekane kuwa hawana haki na ardhi wanayoitumia. Hata inapotokea mwingiliano katika matumizi ya ardhi wanakosa uwezo wa kisheria kukabiliana na uvamizi katika ardhi yao. Huo ni mtazamo wa wakulima juu ya tatizo hilo.

Kwa upande wa wafugaji wao wanaangalia zaidi hati miliki ya ardhi kwa kila mwenye mifugo. Mfugaji anashindwa kuliendeleza au kuhifadhi malisho kwenye eneo ambalo ni la umma. Eneo la kuchungia hutengwa kwa wafugaji wote. Hivyo si rahisi mfugaji kuchukua hatua ya kufuata kanuni bora za ufugaji katika eneo ambalo hana uwezo nalo kisheria.

v. *Ukosefu wa huduma za jamii*

Tatizo hili linawakera zaidi wafugaji. Wafugaji wamejikuta wakilazimika kuingiliana na wakulima kwa vile maeneo mengine ambayo yanatengwa kwa ajili ya ufugaji hayana huduma muhimu kwa jamii kama hospitali, maduka, shule na hasa ukosefu wa mahitaji muhimu ya mifugo kama maji na majosho. Wafugaji hulazimika kufuata huduma hizo wakiwa na mifugo yao hivyo kusababisha mwingiliano katika matumizi ya ardhi na maji.

vi. *Upungufu wa malisho, maji na rutuba*

Wafugaji wanaona kuwa wakati mwingine wanalazimika kuhamisha mifugo yao kufuata malisho. Kwa mfano, wakati wa kiangazi malisho kwenye sehemu zilizotengwa kwa ajili hiyo huwa haba. Wakati huo huo kwenye maeneo ya mashamba huwako mabaki ya mazao na majani yanayofaa kwa malisho. Hata hivyo wafugaji wanaona kuwa hali hiyo imekuwa ni ya kawaida. Wafugaji hufanya makubaliano na wakulima ili walishe mifugo yao baada ya wakulima kuondoa mazao yao shambani. Hata hivyo wafugaji wanakubaliana na wakulima kuwa wapo wafugaji ambao ni **wakorofi** ambao hulazimisha kuchungia kwenye maeneo ya wakulima bila makubaliano. Na wakati mwingine kuingiza kwa nguvu mifugo katika mashamba yenye mazao. Wachungaji wa mifugo wakati mwingine ni watoto wadogo ambao hushindwa kudhibiti idadi kubwa ya mifugo wanayopewa kuangalia wakati mifugo inachungwa kwenye maeneo yenye mazao. Wakati wa kiangazi maji huwa haba. Wafugaji hulazimika kuyafuata maji kwenye maeneo ya kilimo cha mazao ambako pengine huwa kuna mazao ya kiangazi.

Wakulima kwa maoni yao wanaona kuwa upungufu wa rutuba umesababisha wakulima kufungua mashamba maeneo mengine wanayoona kuwa yana rutuba ya kutosha. **Uhaba wa ardhi** huwalazimisha wakulima kufungua mashamba kwenye maeneo ya malisho ili mradi yanarutuba ya kutosha.

Matatizo haya yamesababisha kuwepo kwa **uhamiaji holela**. **Kuongezeka kwa mifugo** pia hufanya wafugaji kuhamishia mifugo yao kwenye maeneo mengine. Wafugaji na wakulima wamekuwa wakihama bila kuangalia kama wanakokwenda utakuweko uwiano sahihi wa shughuli zao na mali asili zilizoko.

### 2.4.2 Matatizo yanayohusu utendaji wa viongozi na serikali

Washiriki wa warsha walibaini kuwa baadhi ya viongozi na watendaji tangu ngazi ya kijiji, wilaya na hata ngazi za juu husababisha kukua kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Serikali pia kwa upande wake ilionekana kuwa inachangia kwa kiasi fulani migogoro hiyo. Matatizo hayo na mitazamo ya washiriki wa warsha juu yake ni kama ifuatavyo:

i. *Haki kutotendeka*

Haki kutotendeka hufanya waathirika kutoamini vyombo vinavyohusika katika usimamiaji wa haki za jamii na matokeo yake ni waathirika kuamua kuchukua sheria mikononi mwao ambazo aghalabu huwa ni mbaya.

Madai ya wakulima ni kuwa mfugaji anapolisha kwenye mazao ya wakulima malalamiko yao hutupwa na viongozi au polisi na kulazimishwa kulipwa fidia ndogo. Hasa pale kesi zinapokwenda polisi au mahakamani maamuzi huwa ni ya kumgandamiza mkulima.

Wafugaji nao wanadai kuwa malipo ambayo hutozwa mfugaji hasa katika ngazi ya kijiji au polisi huwa makubwa kuliko hasara.

ii. *Sheria zilizopitwa na wakati au zisizojitosheleza*

Watendaji na mabwana shamba wanaona kuwa haki inaonekana kutotendeka kwa vile **sheria kuhusu fidia hazieleweki** kwa waathirika. **Sheria zingine zilizopitwa na wakati** kwa mfano fidia ya mazao ya mwaka 1970 thamani yake siyo sawa na ilivyo hivi sasa. Maamuzi yanapofanywa kwa kutumia sheria hizo hutokea kutoridhika kwa upande mmoja. Sheria ya kudhibiti **uhamishaji holela wa mifugo pia haijitoshelezi**. Sheria hiyo inaangalia tu swala la magonjwa na kwamba mhamaji anajulikana na kukubalika anakokwenda. Hali hii imesababisha wafugaji kuhama na mifugo mingi kwenda sehemu ambazo hazimudu kuwa na mifugo kiasi hicho bila migogoro kuwepo.

Washiriki waliona kuwa mianya hiyo ya upungufu wa kisheria hutumiwa na baadhi ya viongozi na watendaji kugandamiza upande wasioupenda.

iii. *Usimamizi hafifu wa sheria na uzembe au uongozi hafifu*

Washiriki wa warsha walikuwa na mtizamo mmoja kuhusu tatizo hilo. Sheria zilizopo hazisimamiwi ipasavyo. Kwa mfano ziko sheria zinazozuia kulima kwenye vyanzo vya maji au kupitisha mifugo kwenye maeneo yasiyohusika. Baadhi ya wakulima na wafugaji wamekuwa wakivunja sheria hizo bila uongozi kuchukua

hatua zozote. Migogoro mikubwa imetokea baada ya kuwepo migogoro midogomidogo ambayo haikuchukuliwa hatua madhubuti.

Baadhi ya viongozi wa siasa pia wamechangia kuwepo kwa migogoro. Viongozi hao wamekuwa wakitetea jamii fulani ama ya wafugaji au wakulima hata kama jamii hiyo inakosea kwa kuhofia kukosa kura kwenye uchaguzi.

iv. *Matumizi mabaya ya amri halali*

Washiriki wa warsha hasa kikundi cha watendaji waandamizi walibaini kuwa amri halali za viongozi zinatumiwa vibaya. Amri halali hutolewa kwa muda maalumu na mazingira maalumu. Lakini imebainika kuwa amri halali inapotolewa huendelea kutumika hata baada ya muda wake kuisha au mazingira yaliyolazimu amri hiyo kutolewa kutokuwepo. Wafugaji au wakulima wameingia katika migogoro wakidai haki kwa kutumia amri halali zilizopitwa na wakati wake.

v. *Migogoro kuwa miradi*

Tatizo hili linawakera zaidi wafugaji. Wafugaji wanaona kuwa baadhi ya wakulima hushirikiana na viongozi au watendaji wa serikali kuchochea migogoro ili wajipatie kipato. Ilidaiwa baadhi ya wakulima hulima kwa makusudi kwenye maeneo ambayo wanajua kuwa lazima mifugo itaingia kuleta uharibifu kama vile kwenye vyanzo vya maji au karibu na njia za mifugo. Mifugo inapoingia kwenye mashamba ya aina hiyo kwa bahati mbaya wenye mashamba hudai fidia kubwa ambayo ikilipwa mwenye shamba anakuwa amepata kipato zaidi ya kile ambacho angekipata kama angeuza mazao yake. Viongozi na watendaji wa serikali hukumbatia hali hiyo kwa masilahi yao pia.

vi. *Rushwa*

Japokuwa haikuwezekana kupata ushahidi wa uhakika kuhusu tatizo la rushwa lakini washiriki wa warsha kwa ujumla walisisitiza kuwa kuwepo kwa rushwa ndiko kunafanya watendaji na viongozi toka ngazi za vijiji, polisi, mahakama na waandamizi wa wilaya kutotimiza wajibu wao kikamilifu. Washiriki pia walijiuliza kama siyo rushwa kwanini watu **wenye uwezo kifedha wanakiburi** cha kufanya wanavyotaka?

vii. *Ukabila*

Kwa mujibu wa wanawarsha ni kuwa hali ya upendeleo kikabila pia inachochea kukua kwa migogoro. Jamii moja inapoona kuwa ina kiongozi wa kuwatetea na jamii nyingine kuona kuwa inakosa haki kwa sababu msimamizi wa kutoa haki hiyo si wa jamii yao.

viii. *Mikakati hafifu ya matumizi ya raslimali kitaifa*

Washiriki waliona kuwa serikali haijaweka mikakati thabiti inayowezesha kuwa na mipango bora na sahihi ya matumizi ya rasilimali kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Kwa mfano haijulikani mifugo inayozidi ipelekwe wapi. Au haijulikani taifa lina uwezo gani kumudu mifugo kiasi gani. Kutokana na hali hiyo serikali haina mikakati ya kuthibiti idadi ya mifugo, hifadhi ya ardhi, malisho na maji.

ix. *Kutohusishwa wakulima na wafugaji na washikadau wengine katika mipango ya maendeleo ya kilimo na mifugo.*

Wanawarsha wote kwa ujumla waliona kuwa serikali imekuwa ikipanga mikakati na mipango ya maendeleo ya kilimo na mifugo bila kuwashirikisha kikamilifu washikadau wote hasa wakulima na wafugaji. Kwa mfano serikali iliamua kuwa vijiji vya wilaya ya Bagamoyo vitengwe vya wakulima wa mazao na vya wafugaji. Wakulima na wafugaji wa wilaya hiyo hawakushirikishwa katika kupanga na kuamua ugawanyaji huo uweje. Matokeo yake vijiji vimegawanywa. Hata hivyo vipo vijiji ambavyo vimepangwa kuwa ni vya wafugaji lakini wapo wakulima ndani yake. Aidha katika vijiji vya wakulima wapo wafugaji ndani yake. Vijiji vingine vinategemea rasilimali muhimu kama maji kutoka vijiji vya jirani na hakuna utaratibu uliowekwa wa namna ambavyo vijiji jirani vitaweza kuchangia matumimizi ya rasilimali ambazo haziko sehemu zote.

### 2.4.3 Matatizo ya kijamii

Washiriki walibaini kuwa pamoja na matatizo yaliyotajwa awali kuwepo, matatizo ya kijamii kwa wakulima na wafugaji katika maeneo ya mogogoro ni kichocheo muhimu katika kukuza migogoro hiyo. Matatizo ya kijamii yaliyoorodheshwa ni:

i. *Kutoheshimu ajira*

Wakulima na wafugaji kila upande unaona kuwa hauheshimu ajira ya mwenzake. Wakulima wanadai kuwa wafugaji hudharau shughuli za kilimo kwa kuona kuwa mazao ni sawa na majani tu hivyo hata kama yakiliwa na mifugo, mwenye mifugo haoni uchungu. Pia wanaona kazi ya kilimo ni ya kimasikini.

Wafugaji pia wanadai kuwa wakulima huona ufugaji kama kazi iliyopitwa na wakati, na kwamba wafugaji wanastahili kukaa porini tu.

ii. *Baadhi ya wakulima kuwaona wafugaji kuwa ni wa kuja*

Wafugaji wanadai kuwa wakulima huwaona wafugaji kuwa ni wahamiaji na kwamba wakulima hujiona wana haki zaidi ya wafugaji katika kutumia rasilimali.

iii. *Tofauti ya mila na desturi*

Wakulima wanadai kuwa desturi ya wafugaji kutembea na silaha huwafanya wawe na kiburi cha kumfanyia mkulima jambo lolote walitakalo. Kwa mfano mfugaji hutembea na sime, fimbo na mkuki. Wanapokutana na mkulima shambani ambaye ana jembe mfugaji humwona mkulima kuwa ni mnyonge na asiye stahili haki. Wafugaji wanadai kuwa kutembea na silaha ni jadi yao na kwa vile wao huchunga mifugo yao porini silaha hizo ni kwa ajili ya kujihami na wanyama wakali.

Wakulima wanadai kuwa jamii za wafugaji hazishirikiani na jamii za wakulima katika misiba. Wafugaji wanadai kuwa wakulima hushiriki katika misiba yao kwa malipo. Ilibainika kuwa wafugaji wa jamii ya kimasai hawana jadi ya kuzikana.

Tofauti hizo za mila na desturi zimesababisha hali ya chuki miongoni mwa jamii zinazohusika kiasi kwamba inapotokea kutofautiana katika jambo lolote chuki hizo huongeza kasi ya mtafaruku.

*iv. Kuwa na mamlaka tofauti katika eneo moja*

Ilibainishwa kuwa kuna vijiji ambako ziko mamlaka au uongozi wa aina tofauti miongoni mwa jamii zilizoko kijijini. Kwa mfano ziko jamii za wafugaji zilizo na mifumo ya kijadi ya uongozi katika vijiji ambavyo vina uongozi wa kiserikali. Hutokea kuwa katika vijiji vya aina hii uongozi wa serikali huwa unatoa maamuzi kwa wanajumuia wote. Lakini uongozi wa kijamii pia hutoa maamuzi kwa ajili ya wanajamii wake japokuwa uamuzi huo unaweza kuwa unapingana na maamuzi ya uongozi wa kiserikali. Hivyo jamii hujikuta zinatekeleza maamuzi tofauti na pia yanayopingana na hivyo kuleta mtafaruku.

*v. Elimu duni ya kilimo na ufugaji bora*

Ilionekana kuwa ukosefu wa utaalamu katika kilimo na ufugaji husababisha matumizi ya rasilimali ya ziada isivyo lazima ambayo husababisha kuingiliana katika matumizi ya rasilimali.

## *2.5 Viini vya matatizo na kipaumbele katika utatuzi*

Kila kundi lililowakilishwa kwenye warsha lilibaini viini vya matatizo yanayosababisha mahusiano baina ya wakulima na wafugaji kuwa mabaya kwa kutumia mbinu ya upembuzi yakinifu. Michoro kwenye Viambatanisho Na. 3 a – d inaonesha kila kikundi kilichowakilishwa jinsi wanavyoona uhusiano wa matatizo yaliyobainishwa, viini vyake na kipaumbele kwa utatuzi wa kila kiini. Matatizo yaliyozungushiwa miduara miwili (ambayo hayana mishale inayoelekea kwayo) ndiyo matatizo viini. Kila kikundi kilitumia kete mia kuzigawanya katika michoro kama inavyoonekana kwenye Viambatanisho 3a – d. Wingi wa idadi ya kete zilizowekwa kwenye kila mduara wa tatizo umeoneshwa kwa namba zilizoko ndani ya miduara. Wingi wa kete unaashiria umuhimu au uzito wa tatizo. Tatizo kiini lenye idadi kubwa ya kete ndilo lililoonekana kuwa linalohitaji utatuzi wa haraka. Kila kundi lililowakilishwa lilionesha uhusiano na kipaumbele cha utatuzi kama ifuatavyo:

### 2.5.1 Kikundi cha wakulima kutoka Doma na Lugoba

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Kutokana na mchoro wa utatuzi yakinifu wa wakulima wa Doma na Lugoba inaonekana kuwa mahusiano mabaya kati ya wafugaji na wakulima yanatokea hasa wanapoingiliana katika matumizi ya rasilimali, wanapohitilafiana sheria, sheria hazisimamiwi vizuri au haki haitendeki katika fidia. Jedwali Na 1. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa wakulima wa kutoka Doma wilaya ya Morogoro vijijini na Lugoba wilaya ya Bagamoyo.

**Jedwali Na. 1: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wa Doma na Lugoba.**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 64 |
| 2. | Sheria zilizopitwa na wakati | 15 |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Mikakati hafifu ya kitaifa katika matumizi ya maliasili | 6 |
| 4. | Vigezo vya fidia kutofahamika | 5 |
| 5. | Uhuru wa wafugaji kutembea na silaha | 5 |
| 6. | Wachungaji wa mifugo (watoto)kutojua majukumu yao | 3 |
| 7. | Chuki za jadi | 2 |

ii. *Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi.*

Matarajio ya wakulima wa Doma na Lugoba: Iwapo matatizo kiini yatatatuliwa kama inavyoonekana katika michoro yao Kiambatisho Na 3a, wakulima hawa wanatarajia kama rushwa haitakuwepo kwa kiasi kikubwa sheria zilizopo zitasimamiwa vizuri na hivyo haki kutendeka kiasi cha kuridhisha. Aidha kwa kiasi kikubwa uongozi utawajibika katika kutenga maeneo vizuri na kwa uwiano sahihi, wakulima na wafugaji watashirikishwa katika mipango ya maendeleo na matumizi ya rasilimali na hivyo kuondoa upungufu wa malisho na hatimaye mwingiliano utapungua.

### 2.5.2 Wafugaji wa Bagamoyo

i. *Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Jedwali Na 2. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa wafugaji wa kutoka wilaya ya Bagamoyo.

**Jedwali Na. 2: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wafugaji wa wilaya ya Bagamoyo.**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Tofauti ya mila na desturi | 25 |
| 2. | Upungufu wa vyanzo vya maji | 20 |
| 3. | Fikira potofu za kuwaona wakulima wa kuja | 15 |
| 4. | Rushwa | 15 |
| 5. | Uhaba wa malisho | 10 |
| 6. | Ukosefu wa mipaka ya vijiji | 10 |
| 7. | Usimamizi dhaifu wa uhamishaji wa mifugo | 5 |

ii. *Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wafugaji wa wilaya ya Bagamoyo wanaona kuwa vyanzo vikuu vya mahusiano mabaya baina ya wakulima na wafugaji ni kuingiliana katika matumizi ya ardhi na kudharauliana. Hivyo iwapo jamii zitavumiliana tofauti zao kimila hali ya kudharauliana haitakuwepo. Pia jamii zitaweka mamlaka zinazoheshimiwa pande zote na hivyo dharau na mwingiliano usio wa lazima katika matumizi ya raslimali hautakuwepo.

### 2.5.3 Wakulima wa Ludewa na Mvumi

i. *Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Jedwali Na 3. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa wakulima wa Ludewa na Mvumi.

**Jedwali Na. 3: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wa Ludewa na Mvumi.**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Serikali kutowajibika | 55 |
| 2. | Rushwa | 21 |
| 3. | Ongezeko la watu | 15 |
| 4. | Tofauti ya mila na desturi | 9 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wakulima wa Ludewa na Mvumi wanaona kuwa vyanzo vikuu vya mahusiano mabaya baina ya wakulima na wafugaji unatokana na kutokuheshimu mipaka. Kutokuheshimiana, uharibifu wa mazao na uharibifu wa ardhi. Wakulima hao wanaona kuwa iwapo serikali itawajibika katika kutoa elimu ya ufugaji bora na kutoa huduma muhimu kwa wafugaji katika maeneo waliyotengewa uhaba wa malisho na uhamiaji holela utapungua. Hivyo mipaka itaheshimiwa, uharibifu wa mazao na ardhi hautakuwepo.

### 2.5.4 Wafugaji wa Morogoro vijijini

*i. Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Jedwali Na 3. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa wafugaji wa kutoka wilaya ya Morogoro vijijini.

**Jedwali Na. 4: Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa wafugaji wa Morogoro vijijini.**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 61 |
| 2. | Uzembe wa viongozi | 16 |
| 4. | Ongezeko la watu na mifugo | 15 |
| 5. | Ukosefu wa huduma za jamii | 8 |

*ii. Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Wafugaji wa wilaya ya Morogoro wanaona kuwa vyanzo vikuu vya mahusiano mabaya baina ya wakulima na wafugaji ni chuki na mapigano yanayotokana na mwingiliano katika matumizi ya raslimali, haki kutotendeka unapotokea mwingiliano, baadhi ya wakulima na wafugaji kuwa wakorofi, na migogoro kugeuzwa miradi na baadhi ya wakulima na watendaji wa serikali.

Kama rushwa haitakuwepo wafugaji hao wanaona kuwa haki itatendeka na hivyo hali ya maridhiano wanapokoseana itakuwepo. Kutokuwepo kwa rushwa kutaondoa jeuri ya wafugaji na wakulima wakorofi. Pia kama viongozi wataacha kuwa wazembe watahakikisha wanapanga vizuri matumizi ya rasilimali zilizopo na kuhakikisha kuwa hakuna ukiritimba katika kutoa haki miliki ya matumizi ya ardhi. Hivyo, mwingiliano katika matumizi ya ardhi hautakuwepo na chuki na mapigano havitatokea.

### 2.5.5 Watendaji waandamizi wa wilaya

i. *Matatizo viini na kipaumbele katika utatuzi*

Jedwali Na 5. linaonesha viini na wingi wa kete zilizowekwa katika kila tatizo kiini kwa mujibu wa watendaji waandamizi wa wilaya.

**Jedwali Na. 5 Matatizo kiini na kipaumbele kwa mujibu wa watendaji waandamizi wa wilaya**

| Na. | Tatizo kiini | Idadi ya kete |
|---|---|---|
| 1. | Rushwa | 57 |
| 2. | Ukosefu wa huduma za kijamii | 10 |
| 3. | Kutokuhusisha washika dau wote katika mipango ya maendeleo | 10 |
| 4. | Tofauti ya uwezo na kiuchumi kati ya wafugaji na wakulima | 10 |
| 5. | Sheria ya kuhamisha mifugo haijitoshelezi na | 10 |
| 6. | Mila na desturi zilizopitwa na wakati | 3 |

ii. *Matarajio kutokana na kipaumbele katika utatuzi*

Watendaji waandamizi wa wilaya wanaona kuwa mahusiano baina ya wafugaji na wakulima yanakuwa mabaya hasa kutokana na mwingiliano katika matumizi ya ardhi, vyombo vya dola kutotenda haki, matumizi mabaya ya amri halali na ukabila.

Washiriki hao waliona kuwa iwapo rushwa haitakuwepo kwa kiasi kikubwa haki itatendeka na amri halali za viongozi zitatumiwa vizuri. Pia viongozi wa siasa watatumia vizuri nafasi zao na ukabila hautakuwa na nafasi.

Kuhusishwa kwa washikadau wote hasa wakulima na wafugaji katika kupanga na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati ya maendeleo utawezesha kuwepo na mipango bora na sahihi ya matumizi ya rasilimali na hivyo kuondoa uhamiaji holela na mwingiliano baina ya wafugaji na wakulima hautakuwepo.

# 3 Mapendekezo ya ufumbuzi, mikakati yake na wahusika katika utekelezaji

Washiriki wa warsha walitoa mapendekezo ya utatuzi wa matatizo viini kulingana jinsi yalivyojitokeza zaidi katika kupewa kipaumbele.

## *3.1 Utatuzi wa rushwa*

Tatizo la rushwa lilipewa kipaumbele na makundi mengi. Mapendekezo ya ufumbuzi yalikuwa ni:

### 3.1.1 Kuboresha mazingira ya watumishi wa serikali

Vitendea kazi, mishahara, makazi na marupurupu ya kazini yaboreshwe ili watumishi wa serikali wasishawishike kirahisi kupokea rushwa na wahamasike kutekeleza wajibu wao.

i. *Watakaowajibika*

Washiriki waliona kuwa serikali pekee ndiyo yenye wajibu wa kurekebisha hali ya mazingira ya watumishi wake.

ii. *Mikakati ya utekelezaji*

Ni wajibu wa serikali kuweka mikakati namna ya utekelezaji wa ufumbuzi huo.

### 3.1.2 Kupanua uelewa wa wananchi juu ya haki zao

Washiriki waliona kuwa wananchi wengi wanalazimika kutoa rushwa au kushawishiwa watoe rushwa kwa kuwa hawaelewi haki zao. Watendaji wenye tamaa ya rushwa hutumia mwanya huo kupoteza haki za watu wasiojua haki zao kwa vile watendaji hao wanajua kuwa waliowapotezea haki zao hawataona haja ya kuzidai au hawaelewi namna ya kuzidai.

i. *Watakaowajibika*

Serikali, wananchi wenyewe na vyama au mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na misaada ya kisheria.

ii. *Mikakati*

- Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali Wahamasishe wananchi kujua haki zao.
- Huduma za kamati za misaada ya kisheria zisogezwe karibu na wananchi.

### 3.1.3 Kukuza uwezo wa wananchi kufuatilia haki zao

Washiriki walibaini kuwa ufuatiliaji wa haki una ukiritimba ambao unahitaji gharama na muda ambao wananchi wengi hawawezi kumudu. Huo pia ni mwanya ambao huwezesha watendaji kupoteza haki za wananchi kwa njia ya rushwa kwa vile wanajua kuwa waliopoteza haki zao hawatakuwa na uwezo kifedha na muda wa kufuatilia haki zao. Hivyo warsha ilipendekeza kuwa uwezo wa wananchi wa kufuatilia haki zao ukuzwe.

i. *Watakaowajibika*

Serikali, wananchi wenyewe na vyama au mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na misaada ya maendeleo.

ii. *Mikakati*

- Serikali ipunguze ukiritimba katika ufuatiliaji wa haki za wananchi. Iweke kanuni zinazoziba mianya inayowawezesha watendaji kusema 'njoo kesho isiyokwisha'.
- Mashirika yasiyo ya kiserikali yawaelimishe wananchi namna ya kuunda vyama vya kusaidiana wanapopata matatizo yanayohitaji fedha na muda.
- Wananchi wawe tayari kuunda vyama vya umoja ni nguvu ili kukabiliana na matatizo ambayo mwananchi mmoja mmoja hawezi kuyamudu.

### 3.1.4 Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa sheria ya rushwa

Washiriki wa warsha walibaini kuwa sheria ya kudhibiti rushwa bado haitekelezwi na kusimamiwa kikamilifu. Hivyo walipendekeza sheria zilizopo za kudhibiti rushwa zisimamiwe na zitekelezwe kwa ufanisi si kwa maneno tu.

i. *Watakaowajibika*

Serikali ndiyo yenye wajibu wa juu.

ii. *Mikakati*

- Serikali ibuni na kuweka mikakati madhubuti

### *3.2 Utatuzi wa kuondoa tofauti za mitazamo ya kimila*

### 3.2.1 Mamlaka za kimila ziondoe tofauti zao

i. *Watakaowajibika*

Wananchi wenyewe

ii. *Mikakati*

Wananchi waunde sheria za kimila zinazokubalika kwa pande zote katika kutatua matatizo yao na kushirikiana kijamii.

### *3.3 Utatuzi wa upungufu wa ardhi malisho na maji kwa ajili ya kilimo na mifugo*

### 3.3.1 Kuhifadhi mazingira

i. *Watakaowajibika*

Wananchi, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na misaada ya kisheria.

ii. *Mikakati*

- Wananchi watumie mbinu endelevu katika matumizi na hifadhi ya maliasili
- Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali watoe elimu sahihi ya matumizi endelevu ya maliasili.
- Serikali ilegeze masharti na iweke mkazo katika kumilikisha ardhi wakulima na wafugaji kwa kulingana na mahitaji yao na uwezo wa maliasili zilizopo.

### 3.3.2 Kuweka uwiano sahihi wa ardhi, maji, mifugo na mazao

i. *Watakaowajibika*

Wakulima, serikali na wataalamu wa fani zinazohusika.

ii. *Mikakati*

- Wakulima watafute na kutumia mbinu sahihi zinazowezesha kuwa na kilimo na ufugaji endelevu bila kuhitaji maji na ardhi zaidi.

- Wataalamu wabuni mbinu sahihi zinazokubalika na kutekelezeka kwa wakulima na wafugaji.
- Serikali isimamie na iwezeshe wataalamu kutimiza wajibu wao.

**3.3.3 Kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua**

i. *Watakaowajibika*

Serikali, wananchi na wataalamu

ii. *Mikakati*

- Wakulima watafute na kutumia mbinu sahihi za uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua kwa ajili ya kilimo na ufugaji
- Wakulima na wafugaji waunde vikundi vya kuvuna, kuhifadhi na kutumia maji ya mvua na yale yatokananyo na vyanzo asili.
- Wataalamu wabuni mbinu sahihi za uvunaji wa maji ya mvua, zinazokubalika na kutekelezeka kwa wakulima na wafugaji.
- Serikali isimamie na iwezeshe wataalamu kutimiza wajibu wao.

***3.4 Ufumbuzi wa mikakati hafifu katika matumizi ya ardhi na maji kwa ajili ya kilimo na mifugo***

**3.4.1 Kuweka mikakati itakayohakikisha matumizi bora na sahihi ya matumizi ya maji na ardhi**

i. *Watakaowajibika*

Serikali ndiyo yenye wajibu mkubwa na wananchi wenyewe

ii. *Mikakati*

- Serikali isimamie ukusanyaji takwimu na kufanya tathmini ya wingi wa mifugo, kiwango cha mahitaji ya ardhi na maji kwa kilimo cha mazao na kujua uwezo wa taifa kwa ufugaji na ukulima wa asili. Kuweka kanuni na taratibu zinazotekelezeka kwa ajili ya upanuzi wa maeneo ya ufugaji au ya kilimo cha mazao kitaifa.
- Ishirikishe wananchi wenyewe katika kupanga na kutekeleza mikakati itakayowekwa.

# 4 HITIMISHO

## *4.1 Tamko la warsha*

Warsha ilitamka kuwa taarifa za kazi za warsha hii iwafikie watendaji wakuu wa Wizara za Kilimo, Maji na Mifugo, na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali ichukue hatua za haraka na sahihi badala ya kungoja mapigano kutokea. Na kwa kuwa migogoro mingi baina ya wafugaji na wakulima ni juu ya matumizi ya ardhi basi Serikali ifanye jitihada za makusudi kusambaza vijitabu vya sheria ya ardhi kwa wananchi na kuwahamasisha kuielewa.

## *4.2 Kufunga*


Warsha ilifungwa rasmi na mgeni rasmi Ndugu Mlanzi, M. M. ambaye ni Afisa Ardhi Wilaya ya Kilosa, wakati wa chakula cha jioni kilichoandaliwa kwa ajili ya kuagana. Mgeni rasmi alisema kuwa aliwashukuru washiriki kwa mchango wao wa mawazo na waandaaji kwa kuhakikisha kuwawezesha washiriki kikamilifu. Alisisitizia washiriki kuhakikisha kufikisha yale waliyoyapata katika warsha hiyo kwa waliowawakilisha na wataalamu kufanyia kazi kikamilifu matokeo ya warsha. Aidha mgeni rasmi aligusia maudhui ya sheria ya ardhi ya jumla Na. 4/99 na ile ya vijiji Na. 5/99 za mwaka 1999 zinazo vipa vijiji mamlaka ya kisheria kuweka mipaka yake na kuwamilikisha ardhi wananchi wake. Mgeni rasmi alidokeza kuwa alifurahishwa kusikia kuwa malengo ya warsha na pia matarajio ya wanwarsha yaliyoorodheshwa siku ya kwanza ya warsha yalifikiwa kwa kiasi kikubwa. Mwisho mgeni rasmi aliwatakia washiriki safarinjeme warudipo makwao. Warsha ilifungwa rasmi saa 2.30 usiku wa tarehe 11 Oktoba 2001.

# Viambatanisho

## Kiambatisho Na. 1: Orodha ya washiriki


| No. | Jina | Jinsia | Anuani |
|---|---|---|---|
| | **Wakulima/wafugaji** | | |
| 1. | Martin Lupatu | me | S.L.P 622, Morogoro |
| 2. | Emanuel Ibrahim | me | S.L.P 622, Morogoro |
| 3. | Hussein Mea | me | S.L.P 622, Morogoro |
| 4. | Omari Shomvi Mtita | me | S.L.P 45, Kimamba Kilosa |
| 5. | Ally M. Mohamed | me | S.L.P Lugoba, Bagamoyo |
| 6. | Onesimo S. Samsindo | me | S.L.P 140, Chalinze |
| 7. | Issa I Mwambala | me | S.L.P 280, Bagamoyo |
| 8. | Shukuru M. Mkali | me | S.L.P Lugoba, Bagamoyo |
| 9. | Juma R. Abdi | me | S.L.P 45, Kimamba, Kilosa |
| 10. | Hamza Damiani | me | S.L.P 173, Kilosa |
| 11. | Safrina R. Simba | ke | S.L.P Mvumi, Kilosa |
| 12. | Morisio Karoli | ke | S.L.P 1880, Doma, Morogoro |
| 13. | Mohamedi Hossen | me | S.L.P Lugoba, Bagamoyo |
| 14. | Pia Leonard | ke | S.L.P Kimamba, Kilosa |
| 15. | Issa A. Mzome | me | S.L.P 1880, Doma, Morogoro |
| 16. | Amina Saidi | ke | S.L.P 45, Kimamba, Kilosa |
| 17. | Bilali M. Msabaha | me | S.L.P 37, Kimamba |
| | **Wataalamu wa ugani** | | |
| 1. | Justin B. Muyobe | me | S.L.P 747, Morogoro |
| 2. | Lemna S. Halfani | ke | S.L.P 81, Chalinze, Bagamoyo |
| 3. | Eleuther Komba | me | S.L.P 747, Morogoro |
| 4. | Lameck E. N. Sitta | me | S.L.P 164 Kilosa |
| 5. | Jackson Mnyeto | me | S.L.P 164, Kilosa |
| | **Watafiti** | | |
| 1. | Laurent A. Kandenuka | me | S.L.P Ilonga, Morogoro |
| 2. | Yakobo N. Msanga | me | S.L.P 5016, Tanga |
| 3. | Cornel L. Rweyemamu | me | S.L.P 3005, Morogoro |
| 4. | Paul Gwakisa | me | S.L.P 3000, Morogoro |
| | **Wataalamu waandamizi** | | |
| 1. | Abihudi Y. Mwasha | me | Afisa mifugo S.L.P 65 Kilosa |
| 2. | Ally N. Ally | me | Mtendaji kata S.L.P 65 Kilosa |
| 3. | Tumbwe S. N. K. | me | Mratibu Nyanda za Malolio S.L.P 65 Kilosa |
| 4. | Mlanzi M. M. | me | Afisa Ardhi S.L.P 133 Kilosa |
| 5. | Joackim Materu | me | Afisa kilimo na Mifugo S.L.P Bagamoyo |
| | **Watayarishaji** | | |
| 1. | Emmanuel Batamuzi | me | S.L.P 3020, Morogoro |
| 2. | Amos Chiligane | me | S.L.P Ilonga Morogoro |
| 3. | Akwilin J.P. Tarimo | me | S.L.P 3035, Morogoro |
| 4. | Joyce Lyimo-Macha | ke | S.L.P 3044, Morogoro |
| 5. | Rodgers E. Malimbwi | me | S.L.P Morogoro |
| | **Mwendeshaji** | | |
| 1. | Amin M. Bakari | me | S.L.P 3236, Morogoro |

# Kiambatanisho Namba 2: Kielelezo cha Mfano Hai wa Ajali Nyingi Barabarani




# Kiambatanisho Namba 3: Michoro inayoonesha uhusiano wa matatizo, viini vyake, na kipaumbele katika utatuzi wa kila kiini


## Kiambatanisho Namba 3 A: Kikundi cha Doma na Lugoba




## Kikundi Namba 3 B: Kikundi cha Bagamoyo



# Kiambatanisho Namba 3 C: Kikundi cha Ludewa na Mvumi



## Kiambatanisho Namba 3 D: Kikundi cha Morogoro Vijijini



## Kiambatanisho Namba 3 E: Watendaji waandamizi

